THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

*MUDA: Saa 2* *Alhamisi 16 Oktoba 2008 mchana*

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote.
3. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

CIVIC EDUCATION TEACHERS' ASSOCIATION



Karatasi hii ina kurasa 8 zenye maandishi.

Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

1. Chagua jibu sahihi katika maswali (i) – (x) kisha uandike herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Katika istilahi ya Kiislamu neno Sunnah lina maana ya
- A kitu kidogo Muislamu anachomfanyia mwenzake
- B jambo la hiari alilofanya Mtume (s.a.w)
- C matendo ya Mtume (s.a.w) ya kiibada
- D mwenendo na mafundisho ya Mtume (s.a.w)
- E simulizi (mapokeo) ya Mtume (s.a.w).

(ii) "*Na anachokupeni mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho*" *(59:7)*. Kwa mujibu wa aya hii umuhimu wa kumfuata Mtume (s.a.w) unaelezwa kama ifuatavyo:
- A Ni agizo la Mwenyezi Mungu
- B Ni miongoni mwa sifa za waja wema
- C Ndio namna ya kumtukuza Mwenyezi Mungu
- D Mtume ndio kiigizo chetu
- E Kumfuata Mtume ni sababu ya kusihi swala zetu.

(iii) Miongoni mwa sababu zilizoongeza msukumo wa hitajio la kukusanya Hadith ni
- A kuzuka Mitume wa uongo
- B kuwepo mashindano ya kuhifadhi Hadith
- C hitajio la kupata rai za maswahaba na makhalifa wanne
- D kupanuka kwa uadui dhidi ya Uislamu
- E hitajio la kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w) kutatua matatizo.

(iv) Uandishi wa Hadith ulishamiri na kufikia kilele wakati wa
- A Mtume (s.a.w)
- B Tabiin
- C Maswahaba
- D Umar bin Abdul Aziz
- E Tabi Tabiin.

(v) Aina kuu mbili za Hadith ni Hadith
- A sahihi na Hadith dhaifu
- B Mutawatir na Hadith Qudusiyyi
- C za uongo na Hadith Hassan
- D Nabawiyyi na Hadith Qudusiyyi
- E Ahad na Hadith al Mash-hur.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

(vi) Kwanini vitabu sita mashuhuri vya Hadith vimeitwa **Sahih Sitta**?

A Vimeandikwa na waandishi waliosafiri masafa marefu kukusanya Hadith
B Waandishi wa vitabu hivyo walijizatiti kuutekeleza Uislamu
C Waaandishi wa vitabu hivi waliishi kipindi cha Tabi Tabiina
D Waandishi wa vitabu hivi walifanya rejea kwenye kitabu mashuhuri cha Imam Malik
E Waandishi wa vitabu hivyo walihakiki Hadith kabla ya kuziandika.

(vii) Miongoni mwa vigezo vilivyotumika kupima usahihi wa Hadith ni

A Hadith ipatikane katika kitabu cha Bukhar
B Matin ya Hadith isipingane na Qur'an
C Hadith iwe na Riwaya zaidi ya moja
D Hadith iwe na isnad na matin
E Kupatikane Hadith nyingine inayofanana nayo.

(viii) Miongoni mwa sababu za kupatikana Hadith za uongo katika karne ya kwanza na ya pili Hijiriyah ni

A fitna ya kugombea ukhalifa
B kukosekana kwa muhadithina
C hapakuwa na sayansi ya uchambuzi wa Hadith
D uandishi wa Hadith ulikuwa katika kiwango kidogo
E hadith hazina ahadi ya kulindwa na Mwenyezi Mungu.

(ix) Kitabu cha Hadith cha Malik Ibn Anas na kile cha Hazarat Ali ni

A Alqatadaya na Al-Muwatta
B Al-Muwatta na An-Nawawi
C Alqatadaya na Sunnan ya Abu Dawd
D Sahih Bukhar na Muslim
E Alqatadaya na sahih Bukhar.

MAKTABA YA SKULI YA NYUKI ZANZIBAR Tarehe ..........

(x) Maana ya Riwaya ni

A isnad ya Hadith moja pamoja na matin yake
B matin ya Hadith Mutawatir yenye isnad iliyokamilika
C Isnad pamoja na matin zote zilizo sahihi
D matin moja inayohadithiwa na Isnad zaidi ya moja
E Hadith mashuhuri iliyopokelewa na Bukhar na Muslim.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

## SEHEMU B: QUR'AN

2. Chagua kutoka orodha B kifungu cha maneno kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka orodha A. Vifungu kutoka orodha B vinaweza kutumika zaidi ya mara moja. Kwa mfano kifungu (i) cha Orodha A kinawiana na kifungu (a) cha Orodha B. **Jibu ni** (i) – (a).

**ORODHA A:**

(i) *"Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba . . . na Mola wako ni Karimu sana (96:1-3).*

(ii) *"Na lau tungekuteremshia maandishi katika karatasi na wakayagusa kwa mikono yao, bila shaka waliokufuru wangesema: Haya si chochote bali ni uchawi dhahiri" (6:7).*

(iii) *"Wala hasemi kwa matamanio (yake). Hayakuwa haya (anayoyasema) ila ni Wahyi uliofunuliwa kwake" (53:3-4).*

(iv) *"Itakapofika nusura ya Mwenyezi Mungu na kushinda ....... Basi hapo mtakase Mwenyezi Mungu pamoja na kumsifu, umuombe maghfira, hakika yeye ndiye apokeaye toba" (110:1-3).*

(v) *"Je, Hakukukuta yatima akakupa makazi? Na hakukukuta hujui kuongoza njia, akakuongoza"? (93:6-7).*

(vi) *"Uteremsho wa kitabu (hiki) umetoka kwa Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu, mwenye hikima" (45:2).*

(vii) *"Tuongoze njia iliyonyooka" (1:6).*

(viii) *"Na mwenye kutenda uovu au akajidhulumu nafsi yake kisha akaomba maghfira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kughufuria na Mwenye kurehemu" (4:110).*

(ix) *"Na ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi) "(6:116).*

(x) *"Lakini makafiri walisema (hayo anayosimulia) ni ndoto zilizovurugika bali ameyabuni mwenyewe... " (21 :5).*

(xi) *"Hawazingatii nini, hii Qur'an? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi" (4 :82).*

(xii) *"Na ikiwa mnashaka kwa haya tuliyomteremshia Mtume wetu, basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake ..."(2 :23).*

(xiii) *"Bali hii ni Qur'an tukufu (iliyotolewa) katika huo ubao uliohifadhiwa, (wa Mwenyezi Mungu)". (85 :21-22).*

(xiv) *"Au ndio wanasema (hivi) kuwa hii (Qur'an) ameitunga (yeye mwenyewe Muhammad) ? Bali wao hawaamini lolote"(52 :33).*

(xv) *"Ewe Mtume ! Mbona (kwa nini) unaharimisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu ! Unatafuta radhi za wake zako (ndio maana ukafanya hivi) ? ..."(66 :1).*

(xvi) *"Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake ; ni Uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu"(2 :2).*


Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

Find this and other free educational resources at http://maktaba.tetea.org

ORODHA : B

(a) Amri ya kwanza aliyopewa Mtume (s.a.w) ni kutafuta elimu kwa ajili ya Allah.
(b) Udhaifu wa madai ya makafiri dhidi ya Qur'an.
(c) *"Ni juu ya Mwenyezi Mungu kuongoza njia iliyosawa" (16:9)*
(d) Qur'an ni ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
(e) Ushindi hutoka kwa Mwenyezi Mungu, hivyo Mja amshukuru yeye na kumuomba msamaha.
(f) Mwenyezi Mungu huwasamehe waja wake kila wanaporejea kwake kikweli kweli.

## SEHEMU C: TAWHIID

Panga vipengele vya (b), (c) na (d) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia. Kwa mfano, Tafsiri ya suratul Ikhlas.

(a) (i) Hakuzaa wala hakuzaliwa
(ii) Mwenyezi Mungu (tu) ndiye anayestahiki kukusudiwa
(iii) Sema: yeye ni Mwenyezi Mungu mmoja (tu)
(iv) Wala hana anayefanana Naye hata mmoja.
**Jawabu ni** :- (a) (iii), (ii), (i), (iv).

(b) (i) Dini anayoiridhia Mwenyezi Mungu ni Uislamu kama Qur'an inavyosisitiza. *"Bila shaka Dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu..." (3:19).*
(ii) Dini ni mfumo wa maisha anaoufuata mwanadamu katika kuendesha maisha yake ya kila siku ya kibinafsi na ya kijamii.
(iii) Uislamu ndiyo dini pekee inayomletea mwanadamu faraja na furaha kwa sababu imetoka kwa Mwenyezi Mungu aliye mjuzi na mwenye hekima.
(iv) Kwa hiyo, dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu haikubaliki kwa kuwa humuelekeza mwanadamu kwenye maisha ya upotevu yenye dhiki na dhulma.
(v) *"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)" 3:85).*

(c) (i) Katika Uislamu Imani ni suala la kutumia akili na kudadisi.
(ii) Kumkanusha Mwenyezi Mungu kunakwenda sambamba na kukanusha kuwepo siku ya malipo.
(iii) Pamoja na miujiza waliyoonesha Mitume, kuna ishara nyingine mbalimbali zinazothibitisha kuwepo Mwenyezi Mungu.
(iv) Miongoni mwa madai ya wanaokana ufufuo ni kuwa haiwezekani mtu kupata uhai baada ya kuoza na mifupa yake kusagikasagika.
(v) Umbile la mbingu na ardhi, nafsi ya mwanadamu na historia yake ni miongoni mwa alama kuu za kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.


Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

(d) (i) Nguzo za imani zimetajwa katika Qur'an: "... *Na mwenye kumkanusha Mwenyezi Mungu na Malaika wake na vitabu vyake na mitume wake na siku mwisho, basi bila shaka amepotea upotofu ulio mbali na haki" (4:136).*

(ii) *"Na katika watu wako wasemao: Tumemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na hali ya kuwa si wenye kuamini" (2:8).*

(iii) Uislamu umejengwa juu ya nguzo za Imani.

(iv) Imani isiyoingizwa katika matendo ya maisha ya kila siku haikubaliki kama inavyosisitizwa katika Qur'an.

(v) Hivyo, imani ya kweli imeelezwa na Mwenyezi Mungu: "*Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha wakawa si wenye shaka, na wakapigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wenye kuamini kweli kweli" (49:15).*

## SEHEMU D : FIQH

4. Jibu kwa ufupi kwa kujaza nafasi zilizo wazi katika swali la (i) – (xv). Andika neno au maneno yanayokosekana tu katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) *"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu" (51:56).*
Kwa mnasaba wa aya hii maana ya "*kumuabudu Mwenyezi Mungu*" ni________.

(ii) Lengo la ujumla la nguzo za Uislamu ni ________________________.

(iii) Kumshuhudia Allah (s.w.) na Mtume Muhammad (s.a.w.) katika shahada ni kuahidi kuwa utaishi kwa mujibu wa ______________ na __________________.

(iv) Tafsiri ya aya inayobainisha lengo la kusimamisha swala ni "____________".

(v) Kutayammamu ni ____________________ kwa kutumia ____________.

(vi) Ambapo **Sijidatus-Sahau** huletwa ili kufidia ____________ iliyosahaulika, **Sijidatul-Tilawat** huletwa baada ya __________________.

(vii) "*Chukua sadaka (zakat) katika mali zao uwatakase kwazo"(9 :103).*
Lengo la zakat ni kuitakasa nafsi ya mtoaji, __________, __________ na uchumi wa jamii.

(viii) Tafsiri ya aya ya Qur'an inayobainisha lengo la swaum ni "______________".

(ix) Kwa mujibu wa Qur'an, miezi ya kunuiya Ibada ya Hija ni __________, _______ na Dhul-Hija.

(x) Matendo ya Hija yanayomtayarisha Muislamu kuwa tayari kupambana na maadui wa Uislamu na kuwa tayari kuua na kuuawa kwa ajili ya Allah ni _______ na _________.

(xi) Aina kuu mbili za talaka ni __________________ na ____________________.

(xii) Kwa mujibu wa Qur'an *Mahari* ni __________________________________________________________.

(xiii) Kwa mtazamo wa Uislamu, mmiliki wa hakika wa mali ni ________ na mwanadamu anamiliki kama ______________________ tu.

(xiv) Sheria ya Kiislamu imegawanya makosa katika makundi yafuatayo :
(a) Makosa ya Hudud (b) ______________ (c) ________________.

(xv) Kwa mujibu wa Qur'an (2:257) mifumo mikuu miwili ya siasa iliyopo ulimwenguni ni:
(a) ____________________________ (b) ________________________.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

## SEHEMU E: TAREKH

Find this and other free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Chagua **neno au kifungu cha maneno** (i)-(xxxii) ili ukamilishe kauli a-p kwa usahihi Mfano, maneno (i) na (ii) yanaifanya kauli (a) kuwa sahihi; **jawabu ni** (a)- (i,ii).

### Maneno au vifungu vya maneno

(i) Udongo
(ii) Asili
(iii) Kimafunzo
(iv) Ibilis
(v) Nuhu (a.s)
(vi) Nasra
(vii) Majini
(viii) Siri
(ix) Uhabeshi
(x) Uwazi
(xi) Kumlaghai
(xii) Kujenga Msikiti
(xiii) Arafa
(xiv) Mayahud
(xv) Fat-hu-Makka
(xvi) Kuunda Ummah
(xvii) Madinah
(xviii) Wanafiki
(xix) Tabuuk
(xx) BAKWATA
(xxi) Kumrubuni
(xxii) Mwezi 9 Dhul-Hija
(xxiii) Uthman bin Affan (r.a)
(xxiv) A.A. Maududi
(xxv) Ali bin Abi Twalib (r.a)
(xxvi) Hassan al-Bannah
(xxvii) Kupigania Uhuru
(xxviii) E.A.M.W.S
(xxix) Kielimu
(xxx) Miaka 950
(xxxi) Subira
(xxxii) Kii-l-hamu

Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

(a) Adam (a.s) ameumbwa kutokana na ....................na mkewe ameumbwa kutokana na ............................hiyo hiyo.

(b) Adui mkuu wa kwanza kwa binadamu ni ......................ambaye ni katika kizazi cha...................................

(c) ..............................ni jina la sanamu lililoabudiwa na watu wa Nabii ............................

(d) Nabii Nuhu (a.s) ni kiigizo cha ................katika kulingania Uislamu. Alilingania watu wake kwa...................................bila kukata tamaa.

(e) Mtume (s.a.w) aliandaliwa..........................kabla ya kupewa Utume na akaendelea kuandaliwa......................mara tu baada ya kupewa Utume.

(f) Katika miaka mitatu ya mwanzo Mtume (s.a.w) alilingania kwa:............., kisha aliamrishwa kulingania kwa...........................................

(g) Kutaka..........................Mtume (s.a.w) na ..........................ni miongoni mwa mbinu walizotumia Makafiri wa Kiquraish dhidi ya Uislamu Makka.

(h) Hijra ya .....................ilikuwa kwa baadhi ya Waislamu ambapo ile ya ..............................ilikuwa kwa Waislamu wote.

(i) ..........................na...........................wa Kiislamu ni baadhi ya mambo ya msingi aliyoyafanya Mtume (s.a.w) katika kuanzisha Dola ya Kiislamu Madinah.

(j) ........................na.....................ni miongoni mwa maadui wakubwa walioibuka dhidi ya Dola ya Kiislamu Madinah.

(k) ........................ na kukimbia vita (kuogopa) kwa Warumi wakati wa Msafara wa ....................ni miongoni mwa matunda ya Mkataba wa Hudaybiya.

(l) Hutuba ya kuaga aliitoa Mtume (s.a.w) ....................katika uwanja wa......................

(m) Baada ya kutawafu Mtume (s.a.w) uongozi wa Dola ya Kiislamu ulienda vizuri mpaka nusu ya kwanza ya uongozi wa Khalifa......................na uliingia katika dosari kubwa wakati wa Ukhalifa wa..............................

(n) Harakati za kuhuisha Uislamu za akina........................wa Misri na ........................wa Pakistani katika karne ya 20 A.D zilitoa mwamko mpya kwa Waislamu.

(o) Waislamu wa Tanganyika walikuwa mstari wa mbele katika..................... kutokana na kunyanyaswa kwao.............................

(p) Baada ya Uhuru Waislamu walianza kwa kasi kubwa kuanzisha shule za Muslim chini ya taasisi yao ya ..........................ambayo baadaye ilivunjwa na kuundwa ..................................

Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner